**HALMASHAURI YA MJI GEITA**

**BARAZA LA WATOTO KATA YA NYANGUKU**

# RISALA YA WATOTO WA BARAZA LA KATA YA NYANGUKU KWA MGENI RASMI KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

**16 /06/2018**

Ndugu Mgeni Rasmi, awali ya yote kwa heshima na taadhima tunakukaribisha sana katika kata yetu ya Nyanguku. Aidha tunakushukuru sana kwa kukubali wito wa kuja kushiriki nasi ukiwa Mgeni Rasmi. Tunajua una majukumu mengi lakini kutokana na Upendo Mkubwa ulio nao kwetu sisi watoto, umeyaacha majukumu na kuja kuungana nasi,Mungu akubariki sana.

Ndugu Mgeni Rasmi, siku ya mtoto wa Afrika huadhimishwa kila mwaka tarehe 16 Juni kukumbuka mauaji ya halaiki ya watoto yaliyofanywa na majeshi ya makaburu katika kitongoji cha Soweto nchini Afrika Kusini mwaka 1976. Watoto hao waliuawa kikatili wakiwa katika maandamano ya kupinga ubaguzi wa rangi kama vile kutumika kwa lugha ya Kiafrikana kuwafundishia watoto wa kiafrika tu ilihali watoto wa kizungu wakitumia lugha ya Kiingereza.

Ndugu Mgeni Rasmi, katika kuadhimisha siku ya mtoto wa Afrika kila mwaka hutolewa kauli mbiu ya kitaifa. Mwaka huu 2018 kauli mbiu ni **"KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA:Tusimwache mtoto nyuma"**

Ndugu Mgeni Rasmi, katika kufanikisha maadhimisho haya ya leo,Baraza la Watoto wa Kata ya Nyanguku kwa kushirikiana na uongozi mzima wa kata na walimu,tumefanikiwa kujadili kauli mbiu ya mwaka huu kwa kuangalia maeneo ambayo mtoto anaweza kushiriki katika kujenga Tanzania ya Viwanda.Kauli Mbiu hii ilijadiliwa katika maeneo makuu matatu ambayo ni Elimu, Afya na Jamii.

Ndugu Mgeni Rasmi, Katika eneo la Elimu watoto tumejadili na kuona kuwa tunaweza kushiriki kwa kupatiwa elimu bora ambayo itatuwezesha kuwa wadadisi,wabunifu na wagunduzi wa vitu mbalimbali kwa uchumi wa viwanda. Katika eneo hili tunawaomba wazazi na jamii kutupa haki yetu ya msingi ya elimu kwa kuandikisha shule watoto kwa wakati bila kuwasahau watoto wenye mahitaji maalum, kuzuia utoro wa rejereja na utoro sugu, kuzuia mazingira hatarishi yanayopelekea mimba na ndoa za utotoni, kutupatia mahitaji yote muhimu ya shule na kushirikiana na walimu pamoja na uongozi wa shule katika kutatua changamoto za kielimu zinazowakabili wanafunzi.Aidha jamii ishiriki kikamilifu katika kuhakikisha shule zetu zina miundombinu stahiki ili kufanya mazingira ya shule kuwa vutivu kwa watoto kujifunza.

Ndugu Mgeni Rasmi, kipekee tunaiomba serikali yetu kuhakikisha shule zetu ambazo zipo pembezoni zinapatiwa huduma ya umeme ili kuwezesha watoto kujifunza kwa vitendo na kutumia teknolojia ya kisasa itakayosaidia kuongeza ubunifu wa watoto

katika kuelekea uchumi wa viwanda. Watoto tunaosoma katika shule za vijijini tunashindwa kujifunza kwa vitendo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutokana na changamoto ya umeme na kukosekana kwa vifaa kama vile kompyuta.

Ndugu Mgeni Rasmi, ushiriki wa mtoto pia katika uchumi wa viwanda unawezeshwa na Afya njema. Katika eneo hili,kwa niaba ya watoto wenzetu wa Halmashauri ya Mji Geita, tumejadili na kuona kuwa watoto wanakabiliwa na changamoto nyingi za kiafya zinazopelekea mahudhurio duni shuleni na wakati mwingine kukatisha masomo na hata vifo.Tunawaomba wazazi kutekeleza jukumu lao la msingi la kuhakikisha tunakuwa na afya njema kwa kutuwahisha hospitali mapema tunapougua au kuonyesha dalili za ugonjwa badala ya kutupeleka kwa waganga wa kienyeji ambao huchelewesha matibabu na kusababisha mtoto kukosa masomo na kuripotiwa kama mtoro.Aidha,tunaiomba serikali yetu itilie mkazo afya ya mama na mtoto kwa kuhakikisha mama zetu wanajifungulia katika vituo vya afya na watoto wanapelekwa kliniki kwa kipindi chote wanachotakiwa ili wapate chanjo stahiki zitakazowawezesha kukua wakiwa na afya njema.Kadhalika huduma ya kwanza iimarishwe shuleni na kutujengea uwezo watoto kujihudumia wenyewe uhitaji unapotokea.

Ndugu Mgeni Rasmi, tutakuwa wachoyo wa fadhila tusipoishukuru serikali yetu ya awamu ya tano chini ya mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuhakikisha watoto tunapata chanjo za kutukinga na maradhi kama vile chanjo dhidi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele(minyoo na kichocho) na chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi. Tunaomba chanjo hizi ziendelee kutolewa kwani mazingira yetu ni hatarishi sana hasa maji tunayoyatumia ambayo sio safi na salama.

Ndugu Mgeni Rasmi, Katika kuimarisha afya ya mtoto, michezo pia ni muhimu sana.Tunawaomba wazazi na jamii kwa ujumla kutupa fursa ya kuonyesha vipaji vyetu vya michezo mbalimbali kwa kutuwekea mazingira mazuri ya kucheza shuleni na hata nyumbani. Tunaomba viongozi wetu wa serikali za vijiji na mitaa kutenga maeneo ya wazi kwa ajili ya watoto kujumuika kwa michezo mbalimbali kuliko kutegemea viwanja vya shuleni tu ambavyo havitoshelezi mahitaji. Aidha, tunaomba msisitizo wa serikali uendelee kuhakikisha wazazi wanachangia tupate chakula cha mchana shuleni ili tuwe na afya njema na kujifunza vizuri.

Ndugu Mgeni Rasmi, katika eneo la jamii, tunaiomba jamii kwa ujumla wake kuhakikisha mtoto anashirikishwa kikamilifu katika uchumi wa viwanda.Jamii ina mchango mkubwa katika hili kwa kuweka mazingira mazuri kwa mtoto kushiriki katika mijadala mbalimbali, kuibua miradi ya maendeleo (watoto tuulizwe kuhusu mahitaji yetu), kutunga sheria ndogondogo hasa zinazomhusu mtoto, kushirikishwa katika ujenzi wa miundombinu ya shule pamoja na usafi na uhifadhi wa mazingira. Aidha tunaiomba jamii itekeleze kwa vitendo kauli mbiu inayosema 'Mtoto wa mwenzako ni mtoto wako' kwa kuhakikisha watoto wote tunakuwa na mienendo mema na kukemea vitendo kama vile watoto kuonekana katika kumbi za starehe (mfano mabanda ya video na disko vumbi) na maeneo hatarishi,ajira za watoto,ukatili wanaofanyiwa watoto majumbani na mitaani,ubakaji na ulawiti.

..gu Mgeni Rasmi, tunaomba pia wazazi na jamii kwa ujumla waelimishwe juu ya ..jibu wao katika malezi ya watoto. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya wazazi wanasahau wajibu wao na kupelekea watoto kuzagaa mitaani na wengine kulelewa katika vituo vya watoto ilihali wazazi wapo lakini hawajitokezi kuwachukua na kuwahudumia watoto wao. Aidha tunawaomba viongozi wetu wa dini kusaidia kutoa semina za ndoa na familia bora ili kuepusha tatizo la wazazi kufarakana na kutengana na mwisho kuwakosesha watoto haki yao ya malezi na hata elimu.

Ndugu Mgeni Rasmi,Tunaomba kuwaasa watoto wenzetu popote walipo kutimiza wajibu wao kikamilifu ili kuondoa migogoro kati yao na wazazi,walezi na jamii inayopelekea wakati mwingine kukoseshwa haki zao za msingi.Aidha, tunawasihi sana watoto wenzetu kuacha tamaa ya fedha na mali ili kutoingia katika mitego ya watu wasiokuwa na nia njema kwa watoto.Tujitahidi pia kutoa taarifa ya matukio ya unyanyasaji na udhalilishaji wa watoto katika vyombo vinavyohusika.Watoto pia tupige vita uzururaji na tabia zinazotupelekea katika mazingira ya hatari ya kubakwa au kulawitiwa. Kadhalika, tuwe wavumilivu, wabunifu, wagunduzi na tuwe na mienendo mizuri na kupenda kubaki katika familia zetu.

Ndugu Mgeni Rasmi, tunawaomba wadau wote na wanaharakati wa haki za watoto wasichoke kutupigania na kuhakikisha tunapata haki zetu kwa ukamilifu. Tunautambua na kuuthamini mchango wao katika mapambano ya haki za mtoto, na kipekee tunayashukuru mashirika ya PLAN International na NELICO ambao wamekuwa karibu nasi wakati wote na kutujengea uwezo katika kutetea na kuzilinda haki zetu. Tunaomba muendelee kuwa karibu nasi, na pia tunazikaribisha asasi zingine ziwaunge mkono katika harakati za kumkomboa mtoto wa Afrika na hasa aliyeko kata ya Nyanguku.

Ndugu Mgeni Rasmi, tutakuwa wachoyo wa fadhila tusipoushukuru uongozi wa kata ya Nyanguku chini ya Mheshimiwa diwani wetu Ndg. Elias Ngole na Afisa Mtendaji wa kata Ndg.George Maguga kwa ushirikiano wanaotupa kama walezi wetu na kuhakikisha baraza linafanya kazi yake.Aidha chini ya uongozi wa viongozi hawa mazingira ya watoto yameendelee kuboreshwa kwa kuhakikisha shule zetu zinakuwa na miundo mbinu stahiki na toshelevu, huduma za afya zinasogea karibu na wananchi ili watoto tusipate tabu na pia kuanzisha harakati za shule yetu ya sekondari ya kata.Tunaomba juhudi zao ziungwe mkono ili kwa pamoja tushiriki katika Tanzania ya Viwanda.

Mwisho Ndugu Mgeni Rasmi, kwa niaba ya watoto wote wa Halmashauri ya Mji Geita,uongozi wa kata ya Nyanguku na wanajamii wa kata ya Nyanguku tunakushukuru sana kuja kujumuika nasi ukiwa mgeni rasmi. Aidha tunawashukuru wageni waalikwa wote mabibi na mabwana kwa kujumuika nasi katika sherehe hii. Na kipekee sana tunaushukuru uongozi wa Halmashauri ya mji Geit kwa kutupa fursa ya kuwa wenyeji wa maadhimisho haya.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Geita - Asanteni sana.**